OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO
SHULE YA SEKONDARI MOROGORO

ANUANI:MKUU WA SHULE
SIMU: +255 689639053
+255 654121607

Shule ya Sekondari Morogoro
S.L.P 240
MOROGORO.

19/05/2021

E-mail: morogorosecondary2018@gmail.com

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na: MSS/ADM/JI/FV/2021

YAH**: KUJIUNGA NA SHULE HII KIDATO CHA TANO 2021/2022**

Napenda kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Morogoro. Ni shule ya Wasichana na Wavulana. Hongera sana kwa kupata nafasi hii.
Umechaguliwa kujiunga na shule hii kwa Masomo Tahasusi ya:
HGL ⬭ **HGK** ⬭ **HGE** ⬭ **HKL** ⬭ **EGM** ⬭
Utakuwa hapa Shuleni kwa muda wa miaka miwili. Kwa kipindi chote utakachokuwa hapa shuleni, tutakuongoza na kukutunza ili uwe na mwenendo wa kufaa. Tunasisistiza Mzazi/Mlezi awe tayari kushirikiana na Uongozi wa Shule katika malezi kwa kutupa taarifa juu ya mwenendo wako ukiwa nyumbani iwapo italazimu.

Kadhalika kila mwisho wa muhula wa masomo tutatuma ripoti ya maendeleo yako ya kitaaluma na kitabia kwa Mzazi/Mlezi wako, tukitegemea kwamba ukiwa nyumbani wakati wa likizo utaendelea kuongozwa. Mzazi au Mlezi tunategemea utatoa ushirikiano wa karibu juu ya mwenendo wa mwamafunzi huyu. Kwa njia hii ya ushirikiano tutaweza kumsaidia mwanafunzi huyu kukua na kuishi maisha bora baadae. Tunasisitiza uwapo shuleni utatakiwa kuweka bidii na juhudi kubwa sana katika masomo ili kufanya vizuri.

Shule ya Sekondari Morogoro ipo Kata ya Boma, Manispaa ya Morogoro, Karibu na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro na mkabala na Kanisa la **KKKT** Usharika wa **Bungo**. Shule ipo umbali wa Kilomita 4 kutoka Kituo Kikuu cha Mabasi cha Morogoro (**Msamvu**). Nauli ya teksi kutoka Msamvu mpaka Shuleni ni kati ya **Tshs.5,000/= na Tsh.6,000/=** tu. Usafiri wa Mabasi madogo (daladala) unapatikana kutoka Msamvu mpaka Mjini kwa **Tshs. 400/=** tu. Tafadhali shukia kituo kikuu cha Mabasi Madogo Mjini kati na panda Pikipiki gharama zake ni **Tsh. 1,000/=,** Teksi / Bajaj ni **Tsh.3,000/=.**

Viambatisho vya Maagizo muhimu vimeambatishwa: **A:** Orodha ya Mahitaji ya Shule, **B**: Sheria za Shule, **C:** Mchanganuo wa Sare za Shule, **D**: Fomu ya Taarifa Binafsi ya Mwanafunzi, **E**: Fomu ya Mzazi/Mlezi , **F**: Fomu ya Hospitali.

BONEPHACE W GONJO

MKUU WA SHULE

MAAGIZO MUHIMU YA KUZINGATIA

Shule itafunguliwa tarehe 05/07/2021 kwa wanafunzi wote. Wanafunzi wa bweni ambao ni wasichana wanatakiwa kuripoti siku moja kabla ya Shule kufunguliwa kabla ya saa 12 jioni. Mwanafunzi afikapo shuleni aripoti Ofisi ya Malezi kwa ajili ya kusajiliwa. Mwisho wa kuripoti shuleni itakuwa ni wiki moja baada ya Shule kufunguliwa, baada ya muda huo nafasi yako itajazwa na mtu mwingine.

Ni muhimu unapokuja Shule ulete Result Slip (Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne 2020) halisi pamoja na Cheti cha kuzaliwa. Hautapokelewa endapo hutawasilisha viambatisho hivi.

A: **MAHITAJI YA SHULE**

SARE ZA SHULE:

Maelekezo kuhusu mshono na aina ya Kitambaa yanapatikana Shuleni**.**

1. Wavulana

- Shati mbili nyeupe za mikono mirefu zenye nembo ya shule
- Suruali mbili zenye uzio chini wa inchi 14. Haturuhusu suruali (**Modal**) zitakatwa kuwa Kaptura kwa mwanafunzi atakayekiuka.
- Raba za Michezo rangi nyeusi
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu na urembo wowote vyenye kamba
- Soksi nyeupe ndefu zisizo na Urembo wowote
- Fulana ya kijivu yenye nembo ya Shule (form six tisheti)
- Sweta la Kijani
- Mkanda wa Suruali mweusi wa ngozi usio na urembo wala mpana zaidi ya sentimita tatu.

2. Wasichana

- Sketi mbili za shule urefu wa inchi 10 toka Miguuni kuelekea kwenye goti.
- Shati mbili nyeupe za mikono mirefu zenye nembo ya Shule
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi visivyo na Urembo wowote vyenye kamba
- Soksi nyeupe ndefu zisizo na Urembo wowote
- Fulana 2 za Kijivu zenye nembo ya Shule (Form six tisheti)
- Sweta la Kijani
- NB: Wsichana wa Kiislamu wanaruhusiwa kuvaa Hijab yenye rangi ya sare ya shule.

USAFI:

Usafi wa Mtu Binafsi:

Ni lazima mwanafunzi awe safi na nadhifu, ***Anyoe Nywele ziwe fupi***. Kucha ni lazima ziwe fupi na bila rangi. Sare ziwe safi na ziwe zimenyooshwa, viatu viwe na hali nzuri na vipigwe kiwi. **SHULE HAIRUHUSU KUSUKA KWA WANAFUNZI WA KIKE.**

Mahitaji ya Darasani

- Mwanafunzi anapaswa kuwa na Madaftari **10** (COUNTER BOOKS QUIRE 2 AU 3)
- Kalamu za risasi za kutosha na vifutio na rula
- Kalamu za kutosha za wino wa bluu au nyeusi
- Ream 2 za Karatasi (**Photocopy A4)** moja (01) na (**Ruled A3**) moja (01). Kabidhi Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa Shule.

MICHANGO NA ADA

1. ADA YA SHULE

Shule yetu ni ya **BWENI** kwa **WASICHANA** na ni ya**KUTWA**kwa **WAVULANA.**

Mwanafunzi wa Bweni ambaye ni Msichana atalipa Tsh. **35,000/=** kwa Muhula au Tsh. **70,000/=** kwa Mwaka. Mwanafunzi wa kutwa ambaye ni Mvulana atalipa **Tsh. 10,000/=** kwa muhula au **Tsh. 20,000/=** kwa Mwaka.

- Kila mwanafunzi anapaswa kuja kiti na meza **(LAZIMA).**
- Lipia fedha za Ada kupitia Benki yoyote ya **NMB** nchinijina la akaunti **Morogoro Secondary School**. Akaunti Namba ya Ada: **22101100145** Fedha **taslimu hazitapokelewa hapa shuleni**.
- Mwanafunzi unatakiwa kuandika Jina lako kamili kwenye Bank Paying Slip (BPS) uliyolipia benki. Endapo atalipa mzazi au mlezi ahakikishe anaandika jina lako na kidato.
- Baada ya malipo wasilisha Bank Paying Slip shuleni kwa Mhasibu wa shule ili kupata risiti ya shule.
- Shule hairuhusu matumizi ya hundi katika kulipa Karo/Ada au kulipia mahitaji mengine.
- Ili kuepuka usumbufu kwa mwanafunzi, mzazi unaombwa kulipa ada katika muda unaotakiwa.

MICHANGO MBALIMBALI

AINA YA MCHANGO	JUMLA	MUHULA WA I	MUHULA WA II
Uzio	*50,000/=*	*50,000/=*	-
Taaluma	*25,000/=*	*15,000/=*	*10,000/=*
Tahadhali	*5,000/=*	*5,000/=*	-
Michezo	*2,000/=*	*2,000/=*	-
Kitambulisho	*4,000/=*	*4,000/=*	-
Ulinzi	*15,000/=*	*15,000/=*	-
Huduma ya Kwanza	*10,000/=*	*10,000/=*	-
Picha za Passport size	*2,000/=*	*2,000/=*	-
Ukarabati wa majengo	*5,000/=*		
JUMLA TSH	***118, 000/=***		

- Michango yote weka kwenye **Akaunti 22101100145, NMB, Morogoro Secondary School.** Nyuma ya benki slip changanua umelipia aina gani ya mchango.

- *Lete Mkononi vifaa vya usafi vifuatavyo**: Dawa ya Chooni Lita 2*** **(**Kati yaLit, Jet, Harpic, Lix Cleaner, Nosa SuperPower, Toilet Bowl Cleaner-BlueTouch) kwa Mwaka. Hatupokei dawa za kutengenezwa nyumbani.

2. SARE ZA SHULE

- Baada ya kuomba wazazi na walezi kushona sare za shule wenyewe, changamoto zilijitokeza za kushona kwa rangi tofauti na ile ya shule lakini pia vipimo havikuwa sahihi. Kwa sasa maelekezo ya kuhusu mshono na kitambaa yanapatikana shuleni.
- Tafadhali usishone sare popote pale ili kuepuka hasara unayoweza kuipata ya kukosea kuchagua rangi ya kitambaa na vipimo vilivyopitishwa na shule.

3. VIFAA VYA KUJA NAVYO WANAFUNZI WA BWENI

(a) Vifaa

- Godoro moja la Futi 2½
- Shuka jozi mbili rangi ya (Bluu Bahari) na Pink (Shuka 2 za Light blue na 2 za Pink)
- Mto mmoja na Foronya mbili za rangi ya Light blue na Pink
- Chandarua cha pembe Nne.
- Blanketi moja
- Mwamvuli au koti la Mvua
- Sahani, Bakuli, Kikombe na Kijiko
- Ndoo ndogo ya lita 10, Kandambili na vifaa vingine kama Mswaki, dawa ya meno
- Kanga, Kitenge na taulo kwa ajili ya kuogea
- Nguo ya kulalia (Night dress)
- Track suit ya rangi ya Light blue/Bluu Bahari
- Sanduku kubwa la bati na Begi dogo la kawaida la kusafiria
- Vitabu vya ibada kwa mujibu wa madhehebu/Dini yako

- **HATARUHUSIWA KUVAA NGUO ZA NYUMBANI** na wala asije nazo **KABISA** hapa shuleni
- Vifaa vingine vya kuja navyo mkononi ni Ndoo **2** ya lita **10** na ya lita **20,** Fagio za Chelewa **3,** Rubber Squeezer **1,** Fyekeo **1,** Brashi ya Mkono **1,** Jembe lenye mpini **1,** Spring faili (siyo plastic) **2**

(b) Matibabu.

- **Shule ina matron mwenye taaluma ya Nursing**. Huduma ya kwanza hutolewa hapa shuleni. Inapolazimu kumpatia mwanafunzi matibabu ya nje ya shule itabidi ahudumiwe hospitali ya Wilaya na Mkoa
- Mwanafunzi apimwe katika **Hospitali ya Serikali** ya Mkoa au Wilaya na kujaziwa Fomu kabla ya kuja.
- Kama utapatikana na **ugonjwa wa kuambukiza** kama **Kifua Kikuu** itabidi utibiwe kabla ya kuja shuleni.
- Iwapo una kitambulisho cha **Bima ya Afya** kitakuwa msaada mkubwa kwako
- kumbuka kuja nacho. Pia Mzazi au Mlezi akupatie fedha za kutosha kwa matibabu
- Tujulishe endapo mwanao ana tatizo la kiafya au ulemavu ambao utahitaji ufahamu wetu pamoja na msaada utakaohitajika.

(C)Usafiri

Shule haitamgharamia usafiri wa kuja shule wala kurudi nyumbani wakati wa likizo. Muhimu mzazi au mlezi kumpatia fedha za nauli Mwanafunzi huyu ajapo shuleni kwa ajili ya usafiri wakati wa likizo. **Shule haitagharamia kumweka shule Mwanafunzi yeyote atakeyeshindwa kusafiri shule ikifungwa**.

B: SHERIA ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya ElimuNa. 25** ya Mwaka **1978.** Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Sheria zote za shule zimewekwa ili kuwawezesha wanafunzi kulifikia lengo la kuwepo kwao hapa shuleni bila matatizo. Aidha sote tunaelewa kuwa nidhamu nzuri huambatana na mafanikio mazuri kitaaluma pia. Hivyo utatakiwa:

- Kuwepo ndani ya mipaka ya Shule muda wote wa masomo na kazi
- Kuhudhuria vipindi vyote vya shule darasani na nje ya darasa, ifahamike kuwa kutoroka vipindi au shuleni ni kosa kubwa
- Kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote wakiwemo walimu wanapoingia dararsani au ukumbi wa mikutano na maeneo mengine wakubwa watakapokuwepo.
- Kutotumia lugha mbaya wakati wote kati yako na wanafunzi wengine au kwa walimu na kwa watu wengine
- Kutovaa vidani kama vile herein, mikufu, bangili, kutotia dawa nywele
- Kutojichora kwa hina au tattoo sehemu ya mwili wako
- Ni lazima kusimama mwalimu aingiapo darasani na kusalimia
- Kutotembelea nyumba za kulala wageni na kumbi za starehe
- Kutokuwa na kucha ndefu na kutopaka rangi au hina
- Wasichana wanatakiwa kukata nywele nusu inchi
- Kuheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wao
- Wavulana hawaruhusiwi kufuga ndevu wala nywele ndefu, nywele zikate nusu inchi. Lugha chafu na Matusi ni Marufuku.
- Kuvaa sare ya shule muda wote wakati wa masomo darasani, nje ya shule kwa shughuli za kishule, anapokwenda hospitali na maeneo mengine
- Kutokuwa na Simu ya Mkononi, SIM Card, Chaja, au Vocha awapo shuleni (Huduma ya simu itatolewa ofisi ya Matron na Mwalimu wa Hostel).
- Kutovaa kofia, jaketi, sweta ambazo siyo la shule
- Kufanya usafi binafsi na wa shule, mazingira na madarasa
- Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
- Kutokwenda nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalumu
- Mafuta yenye harufu kali hayaruhusiwi
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni
- Kuheshimu bendera na wimbo wa Taifa

TANBIHI :

(a) Adhabu kali zitatolewa kwa wanafunzi wote watakaokiuka sheria za shule

(b) **Simu**, **nguo za nyumbani** na vitu vingine visivyotakiwa shuleni vitachukuliwa na havitarudishwa, vyote vitaharibiwa mbele ya wanafunzi wengine.

TARATIBU, NA SHERIA ZA NYONGEZA KWA WANAFUNZI WA BWENI

1. Mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare ya shule muda wote awapo shuleni au bwenini sare isichanganywe na vazi jingine au urembo wowote.

2. Mwanafunzi akishatoka bwenini kwenda shuleni (madarasani) haruhusiwi kurejea tena bwenini pasipo kibali mpaka mwisho wa vipindi.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kupeleka chakula bwenini. Muda wa Chakula uzingatiwe.
4. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki Simu ya Mkononi, SIM Card, Charger, Vocha ya simu awapo shuleni. **HIVYO ASIJE NA SIMU KABISA** endapo itakamatwa itaharibiwa na **mwanafunzi mhusika atafukuzwa shule.**
5. Nguo za Nyumbani haziruhusiwi. Hivyo asije nazo shuleni, anapokuja kuripoti shule avae sare ya shule alikotoka.
6. Mwanafunzi hataruhusiwa kutembelewa na mgeni yeyote bila ruhusa mwalimu wa zamu na mkuu wa bweni. Mgeni awe ni yule aliyeandikwa na mzazi kwenye kumbukumbu za shule. Aidha, si ruhusa mwanafunzi kumpeleka mgeni bwenini.
7. Mwanafunzi akipewa ruhusa ya kwenda kwenye ibada siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili analazimika kurudi shuleni mara baada ya ibada. Si ruhusa mwanafunzi kupitia sehemu nyingine na awe kwenye sare ya shule.
8. **‘’Shoping Day’’** na **‘’Visiting Day’’** zitatangazwa na Mkuu wa shule kwa kushirikiana na Mkuu wa bweni inapolazimu kufanya hivyo. Mwanafunzi atatembelewa siku za Mahafali na Mkutano wa wazazi tu.
9. Si ruhusa mwanafunzi kuwasiliana na ndugu yeyote bila uongozi wa shule kufahamu. Aidha, mwanafunzi atatakiwa kwenda ofisi ya **‘’Matron’’** na **Mkuu wa bweni** ili kutoa shida yake, namba ya simu anayepigiwa na uhusiano wake na mtu atakayepigiwa simu.
10. Ruhusa ya kutoa nje ya shule itatolewa na mwalimu wa malezi kwa kushirikiana na mwalimu wa zamu wa wiki hiyo kwa kutoa kibali maalum cha maandishi na kujisajili kwenye daftari la ruhusa za kutoka nje. Anaporudi ni lazima aripoti ofisi husika.
11. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya mipaka ya shule au bweni bila sababu au kibali maalum atakuwa ni mtoro na atapewa adhabu ya kufukuzwa shule.
12. Si ruhusa kwa mwanafunzi mgonjwa kulala bwenini, atapaswa kulala kwenye chumba maalumu cha wagonjwa **(‘’Sick Bay’’)** kwa kibali cha matroni.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji, Ushoga na Ulawiti
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yoyote ya kulevya
4. Makosa ya jinai
5. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, mwalimu au mtumishi asiye mwalimu
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine
7. Kudharau bendera na wimbo wa Taifa
8. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
9. Kutoa au kushawishi kutoa mimba
10. Kuoa au Kuolewa
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni
12. Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu
13. Utoro(kukaa nje ya shule bila taarifa kwa zaidi ya siku **90)**
14. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani shuleni
15. Kuwa na SIMU ya mkononi, SIM CARD, CHAJA, VOCHA shuleni au bwenini
16. Kutembelea nyumba za kulala wageni, kumbi za starehe, baa, klabu na sehemu zingine ambazo kisheria mwanafunzi haruhusiwi.
17. Usagaji
18. Kujihusisha na Ugaidi

Wanafunzi hawaruhusiwi kabisa kuja na vifaa vilivyoorozeshwa hapa chini. Shule itavichukua na kuviteketeza mbele ya wanafunzi wote.

- Simu ya Mkononi, SIM Card (Laini), Chaja (asije navyo **KABISA** shuleni)
- Radio za aina yoyote
- Pasi ya Umeme.
- “Heater”.
- Kamera.
- Vyakula vya aina yo yote
- Vileo vya aina yo yote.
- Nguo binafsi na Viatu mbali na Sare ya Shule.
- Vidani (Mkufu, Pete, Hereni, Shanga, Vipini n.k.)
- Mikoba yenye mapambo

MWISHO:

Nachukua nafasi hii kukukaribisha Shule ya Sekondari Morogoro na ni matarajio yangu

kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyopewa na Taifa lako.

BONEPHACE W GONJO

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MOROGORO

D: FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

JINA LA MWANAFUNZI: ……..……..……

- TAREHE YA KUZALIWA: ……..
- MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA/WILAYA)……...……..……
- MNAISHI/MNAKAA WAPI?……...(KATA / MTAA) ……
- URAIA: MTANZANIA / SIYO MTANZANIA …….……..…….
- SHULE ALIYOTOKA (KIDATO CHA NNE) …….……....
- ANAHAMIA TOKA SHULE:……..……...
- NAMBA YA MTIHANI (CSEE): ……..……
- PREM NAMBA (WAHAMIAJI):…….……..

TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

- JINA LA MZAZI/MLEZI: ……..…….
- KAZI YA MZAZI/MLEZI: ……..…
- ANUANI YA MZAZI/MLEZI: …….……..….
- SIMU YA MZAZI/MLEZI, KAZINI: ……
  - NYUMBANI: ……MKONONI: …….……..
  - AU KAMA HUNA: JE NAMBARI YA SIMU YA JIRANI YAKO NI:

    ……
- BARUA PEPE (E-mail) YA MZAZI/MLEZI……..

KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA:

Mimi: ……..... Kidato: …… Mwaka: ……..……

Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa naahidi kuyazingatia.

Tarehe: …… Saini..……

B: **KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:**

MWANAFUNZI:

Mimi …… nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na Walimu na Viongozi wote wa Shule, nikikiuka sheria hizo, hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe: …… Saini: …….……..…

E: MZAZI / MLEZI (Ajaze Sehemu hii)

Mimi Mzazi/Mlezi wake nathibitisha kuwa Mwanangu……...ameelewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni…… Madhehebu lake ni……

Ninaruhusu / Siruhusu mwanangu kushiriki katika Makongamano au Warsha za Kidini nje ya shule hususani zile zinazofanyika nje ya Mkoa wa Morogoro pasipo kuwa na Mwalimu Mlezi wa Shule hii

Ninaruhusu / Siruhusu wakati wa Likizo fupi atoke shuleni na kwenda kwa……Uhusiano wake na Mwanangu ni……...

Namba yake ya Simu ni……...

Aidha, mimi……. ambaye ni Mzazi / Mlezi, nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi…… na ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule

…… …….. …..……

Jina La Mzazi/Mlezi Sahihi Ya Mzazi/Mlezi

…….

Tarehe

F: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To The Medical Officer, ….……..

(Name in full)

Please examine the above named student as to her /his physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following categories (i-x)

(i) Eyesight (ii)Hearing (iii) Speech (iv) Limbs (v) Venereal diseases (vi) Leprosy (vii) Epilepsy (viii) Neurosis (ix) Other serious diseases e.g. Asthma, T.B. etc. (x) Pregnancy for girls only.

Name:……..……Date……Signature……

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer). I have examined the above named student and consider that he is fit/unfit for full time studies.

a) Eyesight……

b) Hearing…….....……

c) Speech……

d) Limbs……..……

e) Venereal disease……..……

f) Leprosy……
…

g) Epilepsy……

h) Neurosis…….……

i) Other serious diseases e.gAsthma: ……...
j) Tuberclosis (TB)……..…
k) Pregnancy for girls only…….…..…

OtherComments:
……

Name……**Date**:……..….S**ignature**:……

STATION……**DESIGNATION……**……
…

N.B. I request this form to be returned to the school in a sealed envelope

MOROGORO SECONDARY SCHOOL

A-LEVEL BOOKS REQUIREMENTS

GEOGRAPHY PAPER I:

(i) Monk House (1975). Principles of Physical Geography
(ii) Msabila DT. A comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School
(iii) John Pritchard (1990). Practical Geography for Africa.
(iv) Colin Buckle (1978). Land forms in Africa: An Introduction to Geomorphology.
(v) Bunnett, RB (2014). General Geography in Diagrams.
(vi) Francis Mnyawi(2014). Practical Geography for A-Level
(vii) David Waugh. An Integrated Approach to Geography.
(viii) D.N. McMaster. Map Reading for East Africa.

GEOGRAPHY PAPER II:

(i) Goh Cheng & Morgan. Human and Economic Geography
(ii) Tanzania Institute of Education. Advanced Level Geography Course book
(iii) Msabila, D.T (2014). An Integrated Regional study on Human and Economic Geography

ENGLISH LANGUAGE 1

(i) Asheli, N.E. A Practical Approach
(ii) Kadeghe, M. An Introduction to Language Advanced Level.

ENGLISH LANGUAGE 2

A. **NOVELS AND SHORT STORIES**:

(i) Chinua Achebe: A Man of the people.
(ii) Ayi Ewei Armah: The Beautiful ones are not yet Born.
(iii) Sago: His Excellency the Head of state.

B. **PLAYS:**

(i) Ngungi wa Thiong'o & Ngungi wa Mirii: I will marry when I want by
(ii)H. Ibsen: An Enemy of the people.
(iii)B. Bretch: The Caucasian Chalk Circle.
(iv)F. Imbuga: Betrayal in the City.
(v) Not Yet Uhuru
(vi) I Rwanda Magere
(vii) Black Mamba

C. **POETRY**:

(i) Tanzania Institute of Education: Selected Poems.
(ii) David Cook et. Al: Poems from East Africa

HISTORY:

(i) Rodney W., How Europe Underdeveloped Africa: Nairobi Heinemann Kenya (1992).
(ii) Nyirenda, H.D. Africa in World History. A-Level Certificate Notes DSM (DUP) 1992.
(iii) Nabudere, D.W. Essays on the Theory and Practice of Imperialism. DSM, THP (1979).
(iv) Lenin, V.I.(1982: Imperialism the highest stage of capitalism Moscow, Progress Publishers.
(v) Nyangwine, N. Advanced Level – History Notes, selected Topics for paper 1 & 2. (2002).
(vi) Fr. Jovitus F. Kimara Mwijage, Major Events in African History (2015)

ECOMOMICS 1& 2

(i) R. Mudida. Modern Economics

(ii) Chingan. Principles of Economics
(iii) Drived. Principles of Economics
(iv) Asheck Hussein. A Text Book of Economics.

KISWAHILI 1
(i) Mbunda. Historia ya Kiswahili
(ii) Msokile (1992): Educational Publishers and Distributors Ltd, Dar es Salaam
(iii) Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1958): Kiswahili Sekondari
(iv) James S. Mdee (1988): DUP
(v) Oxford University Press (2012): Kiswahili Kidato cha Tano na Sita.

KISWAHILI 2
(i) Senkoro, F.E.M.K (2011): Fasihi
(ii) TUKI: Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Dar es Salaam. Toleo la Pili.
(iii). Morani. Emmanuel Mbogo. Macmillan AIDAN, DSM
(iv). Kwenye Ukingo wa THim. Ebrahim Hussein

Riwaya
(i) Kufikirika. Shaaban Robert. Mkuku na Nyota Publishers. Dar es Salaam, (2003)
(ii) Mfadhili. Hussein Tuwa. Macmillan AIDAN, (2007)
(iii) Usiku Utakapokwisha. Mbunda Msokile, Macmillan
(iv) Vuta Nkuvute. Shafi A. Shafi, Mkuki na Nyota Publishers, DSM (1999).

Tamthiliya
(i) Nguzo mama. Penina Mhando. Macmillan AIDAN, DSM (2007)
(ii) Kivuli Kinaishi. Said A. Mohamed. Oxford University Press
(iii) Morani. Emmanuel Mbogo. Macmillan AIDAN, DSM.

Ushairi
(i) Mapenzi bora. Shaaban Robert. Mkuki na Nyota Publishers (2007)
(ii) Chungu Tamu. T.A. Mvungi. THP DSM, (2000).
(iii) Fungate ya Uhuru. Mohamed Seif Khatib, DUP, DSM, (2000)
(iv) Kimbunga. Haji Gora Haji. TUKI, DSM (2003)

ADVANCED MATHEMATICS
(i) Septine I. Sillem (2015). Advanced Mathematics For Advanced Secondary Schools Form Five. GDY Publications Ltd. DSM
(ii) Septine I. Sillem (2015). Advanced Mathematics For Advanced Secondary Schools Form Six. GDY Publications Ltd. DSM

Mkuu wa Shule

Mwisho wa Maelekezo

This is just to guide you be aware of Advanced Level books, there are many Authors that you can find in different bookshop